# LAW SCHOOL BULLETIN

Toleo Namba 10 | Oktoba 2022 - Machi 2023

JARIDA LA TAASISI YA MAFUNZO YA UANASHERIA KWA VITENDO (LST)



BODI YA UHARIRI

MKUU WA HUDUMA ZA MAKTABA
Aristarik Maro

AFISA MAWASILIANO
Fatma Salum

LST KUWANOA MAWAKILI KUPITIA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU....................Uk. 1

WAHITIMU SHAHADA YA SHERIA WAHIMIZWA KUJIUNGA NA LAW SCHOOL....................Uk. 4

LST YAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WADAU KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA....................Uk. 6

# LST KUWANOA MAWAKILI KUPITIA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU




***Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud (kushoto) pamoja na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) Mhe. Jaji Imani Aboud (kulia) wakionesha hati za makubaliano ya mashirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo zilizosainiwa tarehe 28 Novemba, 2022 jijini Arusha.***

Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) imesaini makubaliano ya mashirikiano (MoU) na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) kwa lengo la kuendelea kuboresha mafunzo kwa wanafunzi wa uwakili kwenye eneo la haki za binadamu.

Akizungumza mara baada ya kusaini makubaliano hayo tarehe 28 Novemba, 2022 kwenye ofisi za makao makuu ya mahakama hiyo Jijini Arusha, Mkuu wa Taasisi ya LST, Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud aliipongeza mahakama hiyo kwa kuhakikisha haki za binadamu zinazingatiwa katika nchi za Afrika na kuahidi kuendelea kuimarisha jitihada hizo kupitia taasisi yake.

"Naishukuru sana mahakama hii kwani kupitia makubaliano haya wanafunzi wa Law School watapata fursa ya kujifunza zaidi masuala ya haki za binadamu kutoka African Court na wataweza kupata nafasi za kufanya mafunzo sehemu za kazi (field) katika mahakama hii," alisema Mhe. Jaji Masoud.

Aidha alibainisha kuwa makubaliano hayo yataboresha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa LST kwa kuwa yanahusisha kuandaa na kuendesha mahakama za kujifunzia (moot courts) ambazo zitajumuisha wanafunzi kutoka shule za sheria (Law Schools) za nchi za Umoja wa Afrika hivyo wanafunzi wa Tanzania wataongeza uelewa na kupata uzoefu kutoka kwa wenzao wa nchi nyingine kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Naye Rais wa Mahakama hiyo, Mhe. Jaji Imani Aboud alieleza kuwa mashirikiano hayo yatasaidia kuongeza uelewa kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu haki za binadamu na uwepo wa Mahakama ya Haki za Binadamu nchini Tanzania.

## Habari Picha



*Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud (wa tatu kushoto) akitoa neno la shukrani kwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) Mhe. Jaji Imani Aboud (wa nne kutoka kulia) baada ya kusaini makubaliano ya mashirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo jijini Arusha. Wengine ni watumishi wa taasisi hizo.*



*Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud (kushoto), akizungumza na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) Mhe. Jaji Imani Aboud (kulia), baada ya kusaini makubaliano ya mashirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo tarehe 28 Novemba, 2022, jijini Arusha.*



*Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud (kushoto) akimkabidhi zawadi Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) Mhe. Jaji Imani Aboud mara baada ya hafla fupi ya kutiliana saini makubaliano ya mashirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo.*

# MAONESHO YA UTOAJI HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA KWENYE MKUTANO MKUU WA MAWAKILI WA SERIKALI JIJINI DODOMA



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan (wa kwanza kulia) akipata maelezo kuhusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST) kutoka kwa Afisa Sheria wa Taasisi, Farida Jawewa (kushoto katikati) kwenye Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 29/09/2022.***



***Afisa wa Kituo cha Huduma ya Msaada wa Kisheria cha LST, Japhet Kasuka (kushoto), akitoa elimu kwa wadau waliotembelea banda la LST kwenye Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali uliofanyika Jijini Dodoma.***




***Mdau (kushoto), akisoma kipeperushi katika banda la LST kwenye Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali uliofanyika Jijini Dodoma.***

# WAHITIMU SHAHADA YA SHERIA WAHIMIZWA KUJIUNGA NA LAW SCHOOL




***Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (kulia) akizungumza na wanafunzi wa LST Cohort ya 35 waliokuwa wakitoa huduma ya kisheria kwenye banda la Taasisi katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma.***

Serikali imetoa wito kwa wahitimu wa Shahada ya Sheria kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini, kujiunga na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (Law School) ili waweze kupata mafunzo kwa vitendo yatakayowawezesha kufanya kazi zao kwa umahiri na weledi.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro alipotembelea banda la Law School katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika tarehe 22 hadi 29 Januari, 2023 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.
"Ni vyema wahitimu wa shahada ya sheria wakaona umuhimu wa kujiunga na Law School kwa kuwa hawawezi kuwa mawakili au kuajiriwa Serikalini bila kufanya hivyo. Pia hatua hiyo itasaidia kuongeza idadi ya mawakili na mahakimu ambao wanahitajika kwenye maeneo mengi nchini," alisisitiza Dkt. Ndumbaro.

Kwa upande wake Afisa Habari na Mawasiliano wa taasisi hiyo, Fatma Salum ametoa rai kwa wanafunzi wanaojiunga na Law School kuwa na mtazamo chanya kuhusu taasisi hiyo, kuweka juhudi kwenye masomo na kuzingatia nidhamu na hatimaye watafanikiwa kutimiza malengo yao.

Alisema kuwa tangu taasisi hiyo ianze kutoa mafunzo kwa vitendo, zaidi ya asilimia 59 ya wanafunzi waliodahiliwa wamefanikiwa kufaulu mitihani na kuapishwa kuwa mawakili huku wengine wakisubiri kurudia baadhi ya mitihani yao.
"Pia Law School tumeanzisha kozi mpya ya wasaidizi wa kisheria kwa ngazi ya cheti hivyo wale wenye nia ya kutoa huduma ya usaidizi wa kisheria waje kwetu kupata mafunzo ili waweze kusajiliwa, tuna imani baada ya kuhitimu watakwenda kuwasaidia wananchi kwenye masuala mbalimbali ya kisheria pamoja na kutatua changamoto za kisheria katika hatua za awali hasa vijijini ambako bado kuna uhaba wa wanasheria na mawakili," alieleza Fatma.
Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sheria na masuala ya haki huadhimisha Wiki ya Sheria kila mwaka ikiambatana na maonesho ya huduma zinazotolewa na wadau hao. Mwaka huu maadhimisho hayo yalifanyika mkoani Dodoma yakiwa na kaulimbiu isemayo "Umuhimu wa Utatuzi wa Migogoro kwa njia ya Usuluhishi katika Kukuza Uchumi Endelevu. Wajibu wa Mahakama na Wadau."

# TAASISI YA MAFUNZO YA UANASHERIA KWA VITENDO TANZANIA (LST) YASHIRIKI MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA JIJINI DODOMA




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango (kushoto) akizungumza na wananchi katika hafla ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma. Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yalianza tarehe 22 Januari, 2023, katika mikoa mbalimbali nchini na kuhitimishwa tarehe 1 Februari, 2023.*




*Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma (kushoto) akipata maelezo mafupi kuhusu mafunzo yanayotolewa na LST alipotembelea banda la taasisi tarehe 24 Januari, 2023 kwenye maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma. Maonesho hayo yalianza tarehe 22 Januari, 2023 katika mikoa mbalimbali nchini na kuhitimishwa Januari 29 mwaka huu yakifuatiwa na Siku ya Sheria tarehe 1 Februari, 2023.*



*Mdau akiuliza maswali mbalimbali kuhusiana na masuala ya Sheria, alipotembelea banda la LST kwenye Wiki ya Sheria jijini Dodoma*




*Baadhi ya wadau mbalimbali wa masuala ya sheria wakiwemo Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) wakiwa kwenye matembezi ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.*

# LST YAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WADAU KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA

Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika harakati za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud wakati akizungumza kwenye hafla maalum iliyofanyika katika kampasi za LST jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani.

“Hafla hii imeandaliwa na LST kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria,  Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa lengo la kuhamasisha jamii kuungana pamoja ili kupinga ukatili wa kijinsia hasusan kwa wanawake na watoto ambao ndio waathirika wa vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa”, alisema.

Dkt. Masoud alieleza kuwa kutokana na majukumu waliyonayo kisheria, LST ni mdau muhimu katika harakati za kupinga ukatili wa kijinsia kwa sababu inawaandaa mawakili na mahakimu ambao baada ya kuhitimu mafunzo wanatawanyika kwenye jamii kutekeleza majukumu yao ya kusimamia haki katika maeneo mbalimbali nchini na hata nje ya nchi ambako wanakutana na mashauri ya aina tofauti yakiwemo yanayohusu ukatili wa kijinsia.

Aidha alisema kuwa LST inatoa kozi ya Wasaidizi wa Kisheria (Paralegal Program) ambayo imekuja baada ya kuanzishwa sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria (Legal Aid), hivyo kupitia kozi hiyo wanawaandaa Wasaidizi wa Kisheria wenye uelewa wa masuala ya haki za binadamu na ukatili wa kijinsia. Kwa upande wake Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro alieleza kuwa Wizara yake imeanzisha mradi maalumu wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto unaofadhiliwa na GIZ. Kupitia mradi huo mafunzo yatatolewa kwa makundi mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukabiliana na vitendo vya ukatili kwenye mfumo wa haki.

“Tafiti zitafanyika kufahamu mila na desturi zilizopo katika jamii zetu kwa lengo la kuboresha Sheria, Kanuni na Miongozo yetu iendane na misingi ya binadamu. Katika utekelezaji wa mradi huo, wadau wote ni sehemu ya washirika ambao michango yao ya utaalamu na uzoefu itachangia sana kwenye kufikia lengo lililokusudiwa“, alieleza Dkt. Ndumbaro.

Alisisitiza kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau imekua ikifanya juhudi mbalimbali katika kukabiliana na vitendo vya ukatili nchini kupitia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mipango ya kisekta. Baadhi ya juhudi hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008), Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na Kanuni zake, kuanzisha Dawati la Jinsia kwenye Wizara zote, kuanzisha mifumo ya ulinzi wa mtoto katika Halmashauri zote nchini, kuanzisha Dawati la Jinsia na Watoto kwenye vituo vya polisi na kuanzisha mahakama za kusimamia kesi za watoto katika Halmashauri.

Kuanzia Novemba 25 mwaka 2022 nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania zilikuwa katika Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto. Lengo kuu la kampeni hii ilikuwa ni kuongeza uelewa wa jamii ili kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Kampeni hiyo ilihitimishwa Desemba 10, 2022, siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani.




***Msanii wa maigizo kutoka Chuo cha Sanaa Bagamoyo (Tasuba), akifanya tambo za jukwaani kwenye mchezo wa kuigiza ulioonesha vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ambao ulichezwa na wasanii kutoka chuo hicho.***



***Baadhi ya washiriki na wadau mbalimbali waliohudhuria hafla ya maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani iliyofanyika katika kampasi za Taasisi.***

# ZIARA YA NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, MHE. PAULINE GEKUL (MB) KATIKA TAASISI YA MAFUNZO YA UANASHERIA KWA VITENDO



***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Gekul (kulia) akipata maelezo jinsi ya kupata machapisho ya kielektroniki katika maktaba ya Law School (computer lab) kutoka kwa mwanafunzi wa taasisi hiyo (aliyekaa). Wengine pichani ni watumishi wa Taasisi hiyo.***



***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Gekul (kushoto) akimsikiliza Naibu Mkuu wa Taasisi, Prof. Zakayo Lukumay (katikati) kuhusu mfumo wa ufundishaji unaotumika Law School alipotembelea taasisi hiyo juzi jijini Dar es Salaam. Kulia ni mhadhiri aliyekuwa darasani akiwafundisha wanafunzi ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria nchini, Griffin Mwakapeje.***



***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Gekul (kushoto) akiwasalimia wanafunzi wa Law School aliowakuta darasani wakiendelea na masomo.***

# LST YAANZA KUTOA MAFUNZO KWA WASAIDIZI WA KISHERIA



Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (The Law School of Tanzania) imeanza rasmi kutoa mafunzo kwa ngazi ya cheti kwa Wasaidizi wa Kisheria (Paralegals) ili kuwajengea uwezo wa kutoa msaada wa kisheria katika jamii.

Kozi hiyo imepata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET) na mafunzo yameanza rasmi mwezi Novemba, 2022 ambapo yatakuwa yakitolewa kwa muda wa mwaka mmoja katika kampasi za LST na wanafunzi watakaohitimu watatunukiwa cheti (NTA level 4).

Akizungumza katika hafla fupi ya kuwakaribisha wanafunzi wa mwanzo wa kozi hiyo (first batch), Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud alisema kuwa lengo la kuanzishwa kwa kozi hiyo ni kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watu ambao wanafanya kazi kama Wasaidizi wa Kisheria na wanatoa msaada wa kisheria kwa jamii.

“Law School tumeanza kutoa mafunzo haya baada ya Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kukasimu kwetu jukumu la kutoa mafunzo na kusimamia ubora wa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria nchini,” alibainisha.

Aidha aliwataka wanafunzi wa kozi hiyo mpya kusoma kwa bidii na malengo na kuwathibitishia kuwa LST imejipanga vyema kuhakikisha wanapata elimu bora itakayowawezesha kufanya kazi zao kwa umahiri na weledi.

Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 kwa lengo la kusimamia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria pamoja na vyombo vinavyohusika kutoa huduma hiyo kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za sheria nchini ili kuboresha utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii.



# VIKAO VYA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TAASISI YA MAFUNZO YA UANASHERIA KWA VITENDO TANZANIA (LST)



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa LST wakiwa kwenye kikao cha kwanza cha baraza kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kilichofanyika tarehe 28-29 Novemba, 2022 katika ukumbi wa Taasisi jijini Dar es Salaam.*



*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa LST, Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud (kushoto) akichangia hoja kwenye kikao cha baraza kilichofanyika tarehe 28-29 Novemba, 2022 katika ukumbi wa Taasisi jijini Dar es Salaam. Kulia ni Katibu wa Baraza, Ipyana Mwaikambo.*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa LST, wakiwa kwenye kikao cha pili cha baraza kilichofanyika Arusha, tarehe 22 - 24 Februari, 2023.*

# LST YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2023




***Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mhe. Jaji Dkt. Behhajj Masoud (kulia), pamoja na Mhadhiri wa LST, Kisakisa Kiwara (kushoto), wakiwa pamoja na watumishi wanawake wa Taasisi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo mwaka huu imebeba kaulimbiu inayosema "Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu katika Usawa wa Kijinsia".***

Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) imeshiriki kikamilifu katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika tarehe 8 Machi, 2023 kwa lengo la kuendelea kuihamasisha jamii kutambua na kuthamini mchango wa wanawake katika nyanja mbalimbali.

Katika kuadhimisha siku hiyo, Mkuu wa Taasisi ya LST, Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Masoud alitoa rai kwa jamii hasa wanawake kuitumia vyema teknolojia kwa sababu ubunifu na matumizi sahihi ya teknolojia vitasaidia kuondoa vikwazo ambavyo bado wanawake wengi wanakabiliana navyo katika nyanja zote za maisha yaani kijamii, kiuchumi na kisiasa.

"Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inasema kuwa *Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu Katika Kuleta Usawa wa Kijinsia,* hivyo nafasi ya ubunifu na mabadiliko ya teknolojia katika kuleta usawa wa kijinsia ni muhimu sana, hususan, katika kukabiliana na mitazamo ya kibaguzi na vitendo vyote vya unyanyasaji wa wanawake vinavyoathiri jitihada za kuleta usawa wa kijinsia," alisisitiza Dkt. Masoud.

Aidha alibainisha kuwa maendeleo ya teknolojia yanarahisisha kufungua fursa za elimu, ujasiriamali, biashara, uongozi na hata fursa za ajira. Hivyo basi, kwa kutumia teknolojia jamii inaweza kupata taarifa muhimu ambazo zikitumika vizuri zitachangia kuleta fursa sawa na hatimaye kufikia usawa wa kijinsia.

Pamoja na hayo katika kuadhimisha siku hiyo watumishi wanawake wa LST walishiriki kwenye maandamano ya kimkoa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam ambayo yalihitimishwa na sherehe mbalimbali zilizofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja.

Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa tarehe 8 Machi kila mwaka duniani kote kwa lengo la kukumbuka, kutambua, kuthamini na kuenzi jitihada na mchango wa wanawake katika kufanikisha maisha ya kila siku.



# WAZIRI NDUMBARO APOKEA TAARIFA YA KAMATI YA TATHMINI YA MAFUNZO YANAYOTOLEWA NA LST



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa kupokea Taarifa ya Kamati ya Tathmini ya Mafunzo yanayotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST). Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dkt. Harrison Mwakyembe.*



*Mwenyekiti wa Kamati, Dkt. Harrison Mwakyembe, akitoa muhtasari wa Taarifa ya Kamati ya Tathmini ya Mafunzo yanayotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST), kwenye mkutano huo uliofanyika tarehe 20 Novemba 2022, jijini Dar es Salaam.*



*Viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakiwa pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Tathmini ya Mafunzo yanayotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST), kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika kwa ajili ya kukabidhi taarifa ya kamati hiyo.*

# TANZIA

Menejimenti ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) inasikitika kuwatangazia watumishi, wanafunzi na wadau wote wa LST kuhusu kifo cha Prof. John Irving, raia wa Uingereza aliyewahi kufanya kazi na LST katika miaka ya awali ilipoanzishwa. Msiba huo umetokea nchini Uingereza mnamo tarehe 11 Machi, 2023.

Prof. John Irving aliwahi kuwa mkufunzi wa walimu wa LST akishirikiana na mkewe Bi. Johanna Irving. Hivyo, Marehemu alikuwa ni miongoni mwa wadau muhimu wa Taasisi hii kwa kuwa walisaidia kuwapa walimu ujuzi na mbinu za kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo.
Mazishi ya Prof. Irving yamefanyika nchini Uingereza tarehe 06 Aprili, 2023.

LST itaendelea kutambua na kuthamini mchango wao katika kuwawezesha walimu kutoa mafunzo kwa ufanisi.

**MUNGU AIWEKE ROHO YA MAREHEMU MAHALI PEMA PEPONI, AMEN!**
**BWANA AMETOA, NA BWANA AMETWAA, JINA LAKE LIHIMIDIWE!**

Imetolewa na:
Mkuu wa Taasisi
Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania
24 Machi, 2023



Plot No. 2005/2/1 off Sum Nujoma Road, behind Mawasiliano Towers,

PO Box 9422, Dar Es Salaam,

United Republic of Tanzania.

Telephone: +255-22-2927634

Fax: +255-22-2927635

Email: info@lst.ac.tz

Web: www.lst.ac.tz